



88082389



International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 2
SOUAHÉLI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2
SUAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2

Tuesday 4 November 2008 (morning)

Mardi 4 novembre 2008 (matin)

Martes 4 de noviembre de 2008 (mañana)

1 h 30 m

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not turn over this examination paper until instructed to do so.
- Choose one task.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne retournez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Choisissez une tâche.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No dé la vuelta al examen hasta que se lo autoricen.
- Elija una tarea.

Andika maneno yasiyopungua 400 juu ya mojawapo ya haya yafuatayo.

1. Hivi majuzi ulipata fursa ya kuhudhuria mashindano ya kitaifa ya nyimbo za kitamaduni. Ulipendezwa mno na sherehe hizi na ungependa ziendelezwe. Mwandikie barua mhariri wa mojawapo wa gazeti kuu nchini mwako ukielezea yafuatayo: umuhimu wa nyimbo za kitamaduni, na njia mbalimbali ambazo zinaweza kutumiwa kuziendezea.
2. Serikali yako imeanzisha kampeni kabambe za kupambana na ongezeko la baa la njaa nchini. Inadai kuwa “ufanisi bora wa maendeleo nchini unategemea afya bora ya wananchi”. Huku ukitoa mifano, jadili njia nne ambazo zinaweza kutumiwa kupunguza ongezeko la baa la njaa nchini mwako.
3. Shule yako ingependa kuieleza jamii juu ya mipango yake ya kuchangia kwenye maendeleo ya kijamii kupitia kwa miradi midogo midogo ya ukulima. Wewe ukiwa mwenyekiti wa klabu cha ukulima shuleni mwako umeombwa kutoa mchango wako kusaidia shughuli hii. Huku ukitoa mifano, andika makala ambayo yatatolewa kwenye mojawapo wa magazeti nchini mwako juu ya miradi minne midogo midogo ya ukulima ambayo unafikiri shule yako inaweza kushiriki.
4. Hivi karibuni kumekuwa na malalamiko mengi katika jamii yako kuhusu hali mbovu ya shughuli za usafiri na athari zake kwa shughuli za kimasomo kwa wanafunzi wanaosoma kwenye shule za mchana. Wewe ukiwa mmojawapo wa wanafunzi wanaohudhuria shule za mchana umeombwa na mojawapo wa gazeti nchini mwako kufanya mahojiano juu ya hali hii. Andika nakala ya mahojiano yenu.
5. Ili kuwasilisha maudhui yake vizuri ni muhimu kwa mwandishi kufanya uteuzi mwafaka wa wahusika. Ukitumia mifano kutoka kwa mojawapo wa vitabu ambavyo umevisoma darasani jadili maudhui manne yaliyomo kwenye kitabu hicho na ueleze jinsi ambavyo mwandishi amewatumia wahusika mbalimbali kuyafanikisha.
6. Shule yako ingependa kuboresha lishe ya wanafunzi. Wewe kama kiranya msimamizi wa masuala ya chakula shuleni mwako umeombwa na mwalimu mkuu kuyakusanya mapendekezo ya wanafunzi juu ya njia mbalimbali ambazo zinaweza kutumiwa kuboresha lishe shuleni. Andika ripoti ya mapendekezo yao.